JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI INGWE.
S.L.P 136
TARIME
TAREHE .....

NAMBA ZA SIMU
MKUU WA SHULE ***0682-005111***
MAKAMU MKUU WA SHULE ***0753-734147***
PATRON/MATRON ***0762-486270***

MZAZI WA MWANAFUNZI .....
S.L.P .....
.....

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA INGWE HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME – MKOA ,MARA MWAKA 2018/2019
KIDATO CHA TANO

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii ya INGWE mwaka 2018/2019 tahasusi ya HGK/HGL Shule ya sekondari Ingwe ipo umbali wa kilometa 27 kutoka Tarime mjini.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Ingwe ipo mkoa wa Mara Wilaya ya Tarime Tarafa ya Ingwe kata ya Kemambo katika Kijiji cha Kewanja.

Shule ipo kasikazini mashariki mwa mji mdogo wa Nyamongo karibu na mgodi wa Acacia North Mara.

Wanafunzi wanaotoka nje ya wilaya ya Tarime wanapaswa kusafiri na mabasi yaendayo Tarime na kutelemka stendi ya mabasi ya Tarime , hapo uliza magari madogo yaendayo Nyamongo ambapo ni kilometa 27 kufika shuleni. Kwa wale wanaotokea nje ya mkoa wa Mara wanaofikia Mwanza wanapaswa kupanda magari katika kituo cha mabasi cha Buzuruga yapo mabasi maarufu ya ZAKARIA , BATCO ,KISIRI au CHAMPIONI ambayo hufika hadi Tarime mjini.

Shule itafunguliwa muhula wa kwanza tarehe 1/7/2018 kuanzia saa 02:00 asubuhi na mwanafunzi afikapo shuleni aripoti kwa makamu mkuu wa shule kwa mapokezi na usajili. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 15/7/2018baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa. Makamu mkuu wa shule atahakikisha kwamba mwanafunzi amekuja na stakabadhi aliyo lipia A/C **30401200146** NMB BANK, yenye jina la **INGWE SECONDARY SCHOOL RECURRENT AC** pesa zote zinapaswa kulipwa benk na aje na pay inslip.

Shule ina tahasusi (mchepuo) ***HGK*** na ***HGL*** . Kutoka tarime mpaka nyamongo ni shilingi 5000 tu, shuka katika kibao cha shule kabla ya kufika katika stendi ndogo ya nyamongo.

ADA NA MICHANGO YA SHULE

NA	MAHITAJI	MALIPO		JUMLA	AKAUNTI YA BENKI NMB
		MUHULA I	MUHULA II		
1.	KARO	35000	35000	70,000	**30401200146**
2.	MATIBABU	10000		10000	
3	MOCK FM 5 (JOINT)	20,000		20000	
4	TAHADHARI	5000		5000	
5.	UKARABATI WA SAMANI	15000		15000	
6.	KITAMBULISHO NA PICHA	6000		6000	
7.	NEMBO	2000		2000	
8	TAALUMA	20,000		20,000	
9.	ULINZI NA UPISHI	30,000		30,000	
10	REMIDUAL CLASSES	15000		15000	
11	UMISETA	2000		2000	
12	UMEME	20000		20000	

SARE YA SHULE

1. Sketi mbili (zinapatikana shuleni) Rangi ya Idara ya maji kitambaa kizito rinda box) ili kuepuka kuwa na sare isiyofanana rangi pamoja na mshono. Tsh 20,000 kwa kila sketi.
2. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
3. Sweta rangi ya kahawia Tsh 13000. (zinapatika shuleni)
4. Viatu vya ngozi nyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi.
5. Track suit rangi ya blue kwa ajili ya kuvaa usiku.
6. Tisherti light bluee moja (1) zinapatiakana shuleni . Tsh 13,000
7. Shamba dress mbili rangi ya draft bluu na nyeupe (gauni ya kuvaa wakati wa usafi na shughuli za nje) zinapatikana shuleni . Tsh28000 kwa gauni moja. Loso ndefu.
8. Sokisi nyeupe pea mbili (2) ndefu.
9. Tai rangi idara ya maji pea mbili zinapatikana shuleni. Tsh. 3000
10. Kwa waislamu washone juba jeupe



VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI

1. Mathematical set (1)
2. Rula (1)
3. Madaftari makubwa (counter books) yasiyopungua saba (7)
4. Daftari ndogo (4)
5. Kalamu za kutosha

Mzazi / mlezi kumbuka kwamba , ili mwanafunzi aweze kufikia malengo yake ya kitaaluma anapaswa pia awe anasoma vitabu. Unaombwa na BODI ya shule kumnunulia mwanao angalau kitabu kimoja kwa kila somo kulingana na masomo anayosoma katika tahasusi yake. **NI LAZIMA**

MAHITAJI MUHIMU YA KULETA SHULENI.

1. Ream mbili za karatasi za photocopy (DOUBLE A) kila mwaka
2. Godoro la sponge futi 2.5 /6 .
3. Shuka mbili (2) rangi ya pink na bluu.
4. Blanketi na chandaru.
5. Mto na foronya.
6. Ndala / kandambili za kuogea.
7. Kanga.
8. Night dress.
9. Pedi tano (5)
10. Faili moja (1) kwa ajili ya kutunzia kumbu kumbu zake .
11. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vitu vyake (**ni lazima**). Mabegi na masanduku ya thamani kubwa hayaruhusiwi shuleni.
12. Taulo.
13. Ndoo kubwa ya kuchotea maji lita 20.
14. Ndoo ndogo ya kutunzia maji ya kunywa lita 10.
15. Ufagio laini wa ndani (soft bloom) kwa ajili ya kufanyia usafi katika chumba anachoishi.
16. Sahani , bakuli , kijiko na kikombe.
17. Fyekeo/ kwanja moja (1).
18. Reki moja (1)
19. Mfagio mmoja (1) wa nje na squeezer moja (1)
20. Kiwi , dawa ya meno, mswaki na blashi pamoja na toilet paper tano(5).
21. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
22. Cheti cha daktari (kwa wale wenye matatizo ya kiafya)
23. Picha nne za ndugu ama wazazi watakao ruhusiwa kumtembelea mwanafunzi siku za kuwatembelea wanafunzi shuleni (visting day) ambayo ni kila juma pili ya mwisho wa mwezi.
24. Dawa ya choo

MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi.
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake , walimu, walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
6. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
7. Kufuga ndevu.
8. Ulevi ama unywaji wa pombe na madawa ya kulevya.
9. Uvutaji wa sigara.
10. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja , kuoa au kuolewa.
11. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
12. Kushirki matendo ya uharifu , siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
13. Kudharau bendela ya Taifa.
14. Kufanya jaribio la kujiua , au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
15. Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi.

VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
ii. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika mgomo , fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi kukiri maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
iv. Picha (4) za wazazi na ndugu wa kalibu wa wanafunzi wanao weza kutembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
v. Cheti cha kuazaliwa nakala moja.
vi. Result slip.
vii. Cheti cha ugonjwa.

MUHIMU

a. Nguo zote za kiraia haziruhusiwi kabisa kuvaliwa shuleni , hivyo basi mwanafunzi asije nazo shuleni kabisa.
b. Mwanafunzi harusiwi kabisa kuwa na simu ya mkononi / kiganjani shuleni. Akija na simu na akakamatwa , atalipia faini ya Tsh. 50,000/= ili bodi ya shule na kamati ya nidhamu kuhitisha kikao cha kumjadili mwano na kufukuzwa shule.
c. Mzazi / mlezi hakikisha mwanao anapimwa afya yake kikamilifu katika hospitali ya serikali na siyo vinginevyo. Ukifanya udanganyifu hatutakubali sababu zozote zitakazo tolewa baadae.

Nb : ***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. mwanao aje na pesa ya matumizi na akabidhi kwa Mhasibu.***

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Mwl : HELLENI J. ANDREW
MKUU WA SHULE

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

INGWE SEKONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION

Full name .....

Age ..... Height (in cms) ..... weight (in kgs).....

1. Blood count ..... (red and white) .....
2. Stool examination .....
3. Urine analysis .....
4. Syphils and other V.D .....
5. T.B and Leprosy test .....
6. Eye test .....
7. Ear test .....
8. Chest test .....
9. Abdominal test .....
10. Blood group (very crucial) .....
11. Spleen .....
12. HIV test , postive ..... negative .....(tick where necesary)

Adiditional information e.g physical defect or imperements , infections , chronic or family desease (eg. Sickle cell)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

I ceticify that the above student is fit/is not fit to pursue secondary education

Signature .....

Designation .....

Station .....

Date .....

This form must be returned on reporting day

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI INGWE

HISTORIA / TAARIFA YA MWANAFUNZI.

1. Jina la ukoo ..... Jina la kwanza ..... Jina la kati .....
2. Jina la mzazi / mlezi .....namba ya simu .....
3. Kama ni mlezi uhusiano ..... namba ya simu.....
4. Anwani ya kudumu ya mzazi ama mlezi .....
5. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi .....
6. Mahali mwanafunzi alipo zaliwa: Kijiji cha ..... Kata ya ..... Wilaya ..... Mkoa wa .....
7. Dini ..... dhehebu .....
8. Unaingia kidato cha ..... tarehe /mwaka .....
9. Kutoka shule ya sekondari ..... wilaya ..... Mkoa .....
10. Mzazi / mlezi anafanya kazi ajira /mkulima / biashara .....
11. Ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa habari / taarifa muhimu juu yako
    I. ..... uhusiano ..... namba ya simu .....
    II. ..... uhusiano ..... namba ya simu.....
    III. .....uhusiano .... namba ya simu.....
12. Sifa maalumu kama unazo .....
13. Taarifa za wazazi .....
    i. Wapo wote .....
    ii. Yuko mmoja (taja BABA / MAMA .....
    iii. WOTE WAMEFARIKI .....,(weka alama vema panapo husika)

Nakili kuwa maelezo yaliyopo hapo juu ni sahihi.

....

SAINI YA MWANAFUNZI SAINI YA MZAZI / MLEZI

<u>AHADI YA MWANAFUNZI</u>

Mimi (jina la mwanafunzi) ..... nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga shule hii. Naahidi kufata sheria za shule na taratibu zote zilivyotolewa na zitakazotolewa na uongozi wa shule.

<u>AHADI YA MZAZI / MLEZI</u>

Mimi (jina) ..... ambaye ni mzazi / mlezi wa mwanafunzi .....nimeyasoma mashariti na sheria za shule ya sekondari Ingwe ambako binti wangu amechaguliwa kujiunga. Naahindi kuwa nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia mwema wa Taifa letu.

Tarehe ..... Tarehe .....

Jina la mwanafunzi ..... Jina la mzazi / mlezi .....

Sahihi ya mwanafunzi ..... Sahihi ya mzazi / mlezi .....